TANGAZO LA SERIKALI NA. 362 la tarehe10/05/2024

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA VIWANDA MBEZI YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Viwanda Mbezi ya Mwaka 2024.

Utangazaji wa eneo la upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji(mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango

3. Mipango kina katika eneo lililotajwa chini ya aya 2 itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

*Tangazo la Serikali Na. 362 (Linaendelea)*

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YE563 yenye majira - nukta 522382.241MS, 9257915.227KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.11 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba YE536 yenye majira - nukta 522486.866MS, 9257949.909KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.18 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IPC6 yenye majira - nukta 522543.269MS, 9257779.107KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.11 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba IPC10 yenye majira - nukta 522438.979MS, 9257744.548KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.18 hadi ulipoanzia"

Dodoma
25 April, 2024

JERRY WILLIAM SILAA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*